

Mwanafunzi azindua taulo mpya za kike

MWANDISHI WETU

MWANAFUNZI wa Kitzania, Zyaan Virji (16), amezindua taulo za kike zenye uwezo wa kutumika kwa miaka mitatu hadi mitano.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa taulo hizo mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam, Virji ambaye ni kijana wa kiume na mwanafunzi wa Shule ya Aga Khan, alisema sababu zilizomsukuma kutoa taulo hizo ni kutokana na uuzwaji ghali wa taulo zingine za kike. Alisema katika tafiti alizofanya idadi kubwa ya wanawake wanaoishi maeneo ya vijijini wamekuwa wakipata shida wakati wa hedhi hasa kwa wanafunzi ambao baadhi wamekuwa wakishindwa kuhudhuria masomo kutokana na hali hiyo.

Alisema kutokana na bidhaa hiyo kuuzwa kwa bei ya ghali, aliamia kuzindua taulo ambazo zitakuwa na bei ya chini na zitakuwa na uwezo wa kudumu kwa kipindi kirefu na kumfanya mtu yeyote kuwa ana uwezo wa kununua.

Katika harakati za kutengeneza taulo hizo za kike ambazo bado hazijapewa jina, Virji alifanya tafiti katika shule mbalimbali juu ya manunuzi yake ambapo tafiti ilimuonyesha kuwa asilimia mbili ya wanafunzi ndio wenye uwezo wa kumudu kujinunulia taulo za kike.

Aliongeza taulo hizo zitauzwa kwa Sh. 12,000 hadi 15,000 ambapo mnunujaji atajipatia taulo, sabuni pamoja pedi nane na atakapomaliza anaweza kuzisafisha na kurudia tena kuzitumia.

Mgeni rasmi katika uzinduzi huo, Naibu Waziri wa zamani wa Maendeleo, Wanawake, Jinsia na Watoto, Shamim Khan, alimpongeza Virji kwa kubuni kitu kama hicho na kuwataka vijana wengine kuiga mfano huo.

Alitoa mwito kwa jamii ya watu wa Kihindi kutojitenga na jamii nyingine, kwani kwa kufanya hivyo watahindwa kushirikiana katika mambo ya kimaendeleo na ya msingi.